WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TAASISI YA ELIMU TANZANIA

MUHTASARI WA SOMO LA ANATOMIA, FIZIOLOJIA NA PATHOLOJIA YA JICHO FANI YA ULEMAVU WA UONI ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-839-6

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773 005/ +255 222 771 358
Faksi: +255 222 774 420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Muhtasari wa Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa Mwalimu Tarajali Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Idhini

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kumuandaa mwalimu tarajali kuwa mahiri na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa weledi. Mwalimu huyo atafundisha katika shule za msingi zinazodahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mwalimu tarajali atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhitimu mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu na kufaulu mafunzo ya nadharia na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Muhtasari huu umeidhinishwa kuwa ni wa somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
Dodoma

Simu: +255 262 963 533
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

YALIYOMO

Idhini iii

1.0 Taarifa za Awali 1

1.1 Utangulizi..... 1

1.2 Muundo wa Muhtasari 1

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari 2

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania..... 2

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 3

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu..... 4

1.8 Malengo ya Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho 5

1.9 Upimaji na Tathmini 6

1.10 Muda wa Mafunzo 7

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo 7

2.0 Maudhui ya Muhtasari 8

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo 8

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo 10

Majedwali

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati 6

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni 8

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni 10

Orodha ya Machapisho 28

1.0 Taarifa za Awali

1.1 Utangulizi

Muhtasari huu wa somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2019. Muhtasari huu unalenga kumjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni aliyedahiliwa katika elimu ya msingi.

Ili kumsaidia mkufunzi, yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali na zana zinazopatikana kwenye mazingira yanayohusika na upimaji ulioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa kwenye muhtasari huu mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyingine tofautitofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya mwalimu tarajali na umahiri unaojengwa.

1.2 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina taarifa za awali na sehemu ya pili ni maudhui ya muhtasari.

Sehemu ya kwanza inajumuisha utangulizi, muundo wa muhtasari, sababu za kuandaa muhtasari, malengo ya elimu nchini Tanzania, malengo ya jumla ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, madhumuni ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, umahiri wa jumla wa mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, malengo ya somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho, upimaji na tathmini na muda wa mafunzo. Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya muhtasari wa somo.

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari

Dira ya elimu na mafunzo inasisitiza kuwapo kwa mwalimu aliye bora kitaaluma na mwenye mbinu mbalimbali za kufundishia na kijifunzia somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kumuandaa mwalimu mwenye ujuzi wa kumfundisha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni katika shule za msingi kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo inayopasa. Mwalimu tarajali wa somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa ajili ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni anahitaji kupata ujuzi wa kuweza kuyatumia vema mazingira yake.

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo makuu ya elimu nchini:

a) kuendeleza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
b) kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;
c) kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;
d) kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;
e) kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji ya kiuchumi;

f) kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
g) kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
h) kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
i) kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yana malengo yafuatayo:

a) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye ulemavu;
b) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kugundua na kubuni mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia;
c) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
d) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
e) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
f) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
g) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya muda wa miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

a) kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
b) kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
c) kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
d) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini, kuwaendeleza na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
e) kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
f) kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
g) kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
h) kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumwandaa mwalimu tarajali aweze:

a) kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
b) kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
c) kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
d) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonavyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuviendeleza;

e) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
f) kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
g) kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
h) kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
i) kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji katika kufundishia masomo ya taaluma;
j) kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
k) kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonavyo.

1.8 Malengo ya Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho

Muhtasari huu wa somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho, una lengo la kumuandaa mwalimu tarajali wa elimu maalumu atakayeweza:

a) kutumia taaluma ya sayansi ya jicho kubaini mahitaji ya mwanafunzi;
b) kutumia taaluma ya sayansi ya jicho kubaini visababishi vya kutoona;
c) kutumia taaluma ya sayansi ya jicho kuchambua hitilafu za jicho; na
d) kutumia maarifa ya mbinu za upimaji kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.

1.9 Upimaji na Tathmini

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahitaji ya mwalimu tarajali wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa kozi ya ualimu. Upimaji tamati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ukiendelea na utakuwa na alama 50. Upimaji huu unahusisha majaribio, kazimradi, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazi kwa vitendo na mtihani wa mwisho wa muhula. Uzito wa kila aina ya upimaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati

Vipengele	**Njia za Upimaji**	**Mwaka**				**Idadi**	**Alama (%)**
		Mwaka wa I		**Mwaka wa II**			
		Muhula wa I	**Muhula wa II**	**Muhula wa I**	**Muhula wa II**		
Taaluma	Majaribio	1	1	1	1	4	10
	Kazimradi	1	-	1	-	2	5
	Kazi binafsi	1	1	1	-	3	5
	Kazi kwa vitendo	1	1	1	-	3	5
	Mkoba wa kazi	1	-	1	-	2	5
	Mtihani wa mwisho wa muhula	1	1	1	-	3	20
Upimaji endelevu							50
Upimaji tamati: Mtihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania					1	1	50
Jumla ya alama za upimaji endelevu na upimaji tamati							**100**

1.10 Muda wa Mafunzo

Muhtasari huu wa somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa fani ya ulemavu wa uoni umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwalimu tarajali misingi muhimu ya maarifa ya somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho itakayomwezesha kumfundisha kikamilifu mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kumudu ujifunzaji katika elimu ya msingi

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo

Maudhui ya muhtasari yamepangwa katika jedwali yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi

1.11.1 Umahiri

Ni uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ufanisi

1.11.2 Umahiri Mkuu

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwalimu tarajali baada ya kujifunza kwa muda fulani. Hujengwa na umahiri mahususi atakaojengewa mwalimu tarajali kwa kutenda shughuli mbalimbali

1.11.3 Umahiri Mahususi

Ni uwezo atakaojengewa mwalimu tarajali katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu

1.11.4 Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali

Ni vitendo ambavyo mwalimu tarajali anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa

1.11.5 Vigezo vya Upimaji

Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwalimu tarajali ili kufikia umahiri mahususi

1.11.6 Viwango vya Utendaji

Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo vya kila shughuli anayotenda mwalimu tarajali

1.11.7 Idadi ya Vipindi

Idadi ya vipindi ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Somo hili litafundishwa kwa vipindi viwili kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

2.0 Maudhui ya Muhtasari

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1.0 Kutumia sayansi ya jicho kubaini mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	1.1 Kuchambua mfumo wa jicho na kazi zake 1.2 Kuchambua mfumo kazi wa uoni katika kubaini changamoto za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 1.3 Kuchambua mahitaji ya ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
2.0 Kutumia sayansi ya jicho kubaini visababishi vya ulemavu wa uoni	2.1 Kutumia taaluma ya uoni katika kujenga dhana ya ulemavu wa uoni 2.2 Kujenga uwezo wa kuchambua magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni 2.3 Kujenga uwezo wa kuchambua visababishi vingine vya ulemavu wa uoni
3.0 Kutumia sayansi ya jicho kuchambua hitilafu katika jicho	3.1 Kutumia sayansi ya jicho kubaini hitilafu za uoni 3.2 Kutumia sayansi ya jicho kurekebisha hitilafu za uoni 3.3 Kutumia sayansi ya jicho kuchambua athari za uoni katika ujifunzaji
4.0 Kutumia mbinu za upimaji katika kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	4.1 Kutumia maarifa ya upimaji kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 4.2 Kutumia vifaa vya upimaji kuchunguza changamoto za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 4.3 Kutumia mbinu za upimaji katika kutoa afua stahiki za kielimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 4.4 Kutoa afua stahiki kwa wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni (kutoa rufaa, kupendekeza huduma kulingana na mahitaji, kurekebisha maeneo, vifaa saidizi na hali)

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Anatomia, Fiziolojia na Patholojia ya Jicho kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
1.0 Kutumia sayansi ya jicho kubaini mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	1.1 Kuchambua mfumo wa jicho na kazi zake	a) Kubaini sehemu za jicho	Sehemu za jicho zimebainishwa.	Anabainisha sehemu za nje za jicho.	Anabainisha sehemu za nje na za kati za jicho.	Anabainisha sehemu za nje, za kati na za ndani za jicho.	Anabainisha sehemu za nje, za kati na za ndani za jicho katika kifani.	8
		b) Kufafanua sehemu za jicho (za nje, za kati na za ndani, kuchora na kuonesha)	Sehemu za jicho zimefafanuliwa.	Anafafanua sehemu za nje za jicho kwa kuchora na kuonesha sehemu zake.	Anafafanua sehemu za nje na za kati za jicho kwa kuchora na kuonesha sehemu zake.	Anafafanua sehemu za nje, za kati na za ndani ya jicho kwa kuchora na kuonesha sehemu zake.	Anafafanua sehemu za nje, kati na ndani ya jicho kwa kuchora na kuonesha sehemu zake na kwa kuhusianisha na mazingira.	
		c) Kuelezea kazi za sehemu za jicho	Kazi za sehemu za jicho zimeelezwa.	Anaeleza kazi za sehemu za nje za jicho.	Anaeleza kazi za sehemu za nje na za kati za jicho.	Anaeleza kazi za sehemu za nje, za kati na za ndani za jicho kwa michoro.	Anaeleza kazi za sehemu za nje, za kati na za ndani za jicho kwa michoro na katika kifani kwa kutumia mazingira halisi.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	1.2 Kuchambua mfumo kazi wa uoni katika kubaini changamoto za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kufafanua dhana ya uoni (maana, aina na umuhimu)	Maana, aina na umuhimu wa uoni vimefafanuliwa.	Anafafanua maana ya uoni.	Anafafanua maana na aina za uoni.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa uoni.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa uoni kwa kutumia mchoro/michoro mguso.	8
		b) Kuchambua njia za mwanga kutoka katika chanzo hadi ndani ya jicho	Njia za mwanga kutoka katika chanzo hadi ndani ya jicho zimechambuliwa.	Anachambua njia za mwanga kutoka katika chanzo hadi sehemu ya nje ya jicho.	Anachambua njia za mwanga kutoka katika chanzo hadi sehemu ya nje na ya kati ya jicho.	Anachambua njia za mwanga kutoka katika chanzo hadi sehemu ya nje, ya kati na ya ndani ya jicho.	Anachambua njia za mwanga kutoka katika chanzo hadi sehemu ya nje, ya kati na ya ndani ya jicho katika mchoro/mchoro mguso.	
		c) Kuelezea mfumo kazi wa uoni	Mfumo kazi wa jicho umeelezwa.	Anaeleza mfumo kazi wa jicho kuanzia kwenye chanzo mpaka sehemu ya nje ya jicho.	Anaeleza mfumo kazi wa jicho kuanzia kwenye chanzo mpaka sehemu ya nje na ya kati ya jicho.	Anaeleza mfumo kazi wa jicho kuanzia kwenye chanzo mpaka sehemu ya nje, ya kati na ya ndani ya jicho.	Anaeleza mfumo kazi wa jicho kuanzia kwenye chanzo mpaka sehemu ya nje, kati, na ndani na jinsi taswira inavyotafsiriwa kwenye ubongo.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	1.3 Kuchambua mahitaji ya ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kufafanua dhana ya mahitaji maalumu	Dhana ya mahitaji maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa uoni imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya mahitaji maalumu.	Anafafanua dhana ya mahitaji maalumu kwa kutoa mifano ya mahitaji ya kundi mojawapo.	Anafafanua dhana ya mahitaji maalumu kwa kutoa mifano ya mahitaji ya makundi yote ya wanafunzi wenye ulemavu wa uoni.	Anafafanua dhana ya mahitaji maalumu kwa kutoa mifano ya mahitaji ya makundi yote ya wanafunzi wenye ulemavu wa uoni na kutaja mahitaji kwa makundi yote.	6
		b) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Mahitaji maalumu ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni yamebainishwa.	Anabainisha hitaji moja (kupata taarifa) kwa mwanafunzi na kutoa mifano.	Anabainisha mahitaji mawili (kupata taarifa na mahitaji ya ujongeaji) kwa mwanafunzi na kutoa mifano.	Anabainisha mahitaji matatu ya (kupata taarifa, mahitaji ya ujongeaji na mahitaji ya vifaa saidizi) mwanafunzi na kutoa mifano.	Anabainisha mahitaji manne ya (kupata taarifa, mahitaji ya ujongeaji, mahitaji ya vifaa saidizi, na mahitaji ya kupata ujuzi wa kuvitumia vifaa saidizi) mwanafunzi na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubaini zana za ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Zanamguso, masikizi, zana za kuona kwa wenye uoni hafifu na za TEHAMA zimebainishwa.	Anabainisha aina moja ya zana za kufundishia na kujifunzia kwa mwanafunzi.	Anabainisha aina mbili za zana za kufundishia na kujifunzia kwa mwanafunzi.	Anabainisha aina tatu za zana za kufundishia na kujifunzia (zanamguso, masikizi na za TEHAMA) kwa ajili ya ujifunzaji wa mwanafunzi na kutoa mifano.	Anabainisha aina nne za zana za kufundishia na kujifunzia (zanamguso, masikizi, zana za kuona kwa wenye uoni hafifu na za TEHAMA) kwa mwanafunzi na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira halisi.	
2.0 Kutumia sayansi ya jicho kubaini visababishi vya ulemavu wa uoni	2.1 Kutumia taaluma ya uoni katika kujenga dhana ya ulemavu wa uoni	a) Kueleza dhana ya uoni (maana na makundi)	Maana na makundi mawili ya wanafunzi wenye ulemevu wa uoni vimeelezwa.	Anaeleza maana na kundi moja la wanafunzi.	Anaeleza maana na makundi mawili ya wanafunzi.	Anaeleza maana na makundi mawili ya wanafunzi na kufafanua kwa mifano.	Anaeleza na kufafanua maana na makundi mawili ya wanafunzi na kuyatofautisha.	8

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuchambua viashiria vya ulemavu wa uoni kwa kuzingatia makundi matatu (tabia, muonekano na malalamiko)	Viashiria vya ulemavu wa uoni kwa kuzingatia makundi matatu (tabia, muonekano na malalamiko) vimechambuliwa.	Anachambua viashiria viwili vya ulemavu wa uoni kwa kuzingatia kundi moja.	Anachambua viashiria vitatu vya ulemavu wa uoni kwa kuzingatia makundi mawili.	Anachambua viashiria vinne vya ulemavu wa uoni kwa kuzingatia makundi mawili na kutoa mifano.	Anachambua viashiria vitano vya ulemavu wa uoni kwa kuzingatia makundi matatu na kutoa mifano.	
		c) Kueleza athari za ulemavu wa uoni	Athari za ulemavu wa uoni kielimu, kijamii, kisaikolojia na kiuchumi zimeelezwa.	Anaeleza athari moja ya ulemavu wa uoni kutoka katika kila kundi.	Anaeleza athari mbili za ulemavu wa uoni kutoka katika kila kundi .	Anaeleza athari tatu za ulemavu wa uoni kutoka katika kila kundi.	Anaeleza athari nne za ulemavu wa uoni kutoka katika kila kundi na kutoa mifano.	
	2.2 Kujenga uwezo wa kuchambua magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni	a) Kufafanua magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni	Magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni yamefafanuliwa.	Anafafanua ugonjwa mmoja unaosababisha ulemavu wa uoni.	Anafafanua magonjwa mawili yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anafafanua magonjwa matatu yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anafafanua magonjwa manne yanayosababisha ulemavu wa uoni na kutoa mifano inayoakisi mazingira halisi.	9

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kueleza athari za magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni	Athari za magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni zimeelezwa.	Anaeleza athari moja ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anaeleza athari mbili za magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anaeleza athari tatu za magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anaaeleza athari nne za magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	
		c) Kueleza tahadhali za kuchukua dhidi ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni	Tahadhali za kuchukua dhidi ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni zimeelezwa.	Anaeleza tahadhali moja ya kuchukua dhidi ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anaeleza tahadhali mbili za kuchukua dhidi ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anaeleza tahadhali tatu za kuchukua dhidi ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	Anaeleza tahadhali nne za kuchukua dhidi ya magonjwa yanayosababisha ulemavu wa uoni.	
		d) Kuchora jicho na kuonesha sehemu zinazoathiriwa na magonjwa	Jicho linachorwa na kuonesha sehemu zinazoathiriwa na magonjwa.	Anachora jicho na mchoro mguso na kuonesha sehemu moja inayoathiriwa na magonjwa.	Anachora jicho na mchoro mguso na kuonesha sehemu mbili zinazoathiriwa na magonjwa.	Anachora jicho na mchoro mguso na kuonesha sehemu tatu zinazoathiriwa na magonjwa na kutoa mifano.	Anachora jicho na mchoro mguso na kuonesha sehemu nne zinazoathiriwa na magonjwa na kutoa mifano.	
		e) Kutengeneza vifani vya jicho na kuonesha sehemu zinazoathiriwa na magonjwa	Ametengeneza vifani vya jicho na kuonesha sehemu kumi zinazoathiriwa na magonjwa.	Anatengeneza kifani kimoja cha jicho na kuonesha sehemu nne zinazoathiriwa na magonjwa.	Anatengeneza kifani kimoja cha jicho na kuonesha sehemu sita zinazoathiriwa na magonjwa.	Anatengeneza kifani kimoja cha jicho na kuonesha sehemu nane zinazoathiriwa na magonjwa.	Anatengeneza kifani kimoja cha jicho na kuonesha sehemu kumi zinazoathiriwa na magonjwa.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	2.3 Kujenga uwezo wa kuchambua visababishi vingine vya ulemavu wa uoni	a) Kueleza visababishi vingine vya ulemavu wa uoni	Visababishi vingine vya ulemavu wa uoni vimeelezwa.	Anaeleza visababishi vingine viwili vya ulemavu wa uoni.	Anaeleza visababishi vingine vitatu vya ulemavu wa uoni.	Anaeleza visababishi vingine vinne vya ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	Anaeleza visababishi vingine vitano vya ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	9
		b) Kubaini makundi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni	Makundi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni yamebainishwa.	Anabainisha kundi moja la visababishi vingine vya ulemavu wa uoni.	Anabainisha makundi mawili ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni.	Anabainisha makundi matatu ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	Anabainisha makundi matatu ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira halisi.	
		c) Kufafanua uhusiano kati ya dhana ya ulemavu wa ngozi (ualbino) na ulemavu wa uoni	Uhusiano kati ya dhana ya ulemavu wa ngozi (ualbino) na ulemavu wa uoni umefafanuliwa.	Anafafanua maana ya ulemavu wa ngozi (ualbino) na ulemavu wa uoni.	Anafanua maana ya ulemavu wa ngozi (ualbino) na uhusiano wake na ulemavu wa uoni.	Anafafanua maana, uhusiano na chanzo cha ulemavu wa ngozi (ualbino) na uhusiano wake na ulemavu wa uoni.	Anafafanua maana, uhusiano, chanzo na athari za ulemavu wa ngozi (ualbino) kuhusiana na ulemavu wa uoni.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kubainisha imani na ukweli kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino)	Imani potofu na ukweli kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino) vimebainishwa.	Anabainisha imani potofu kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	Anabainisha imani potofu na ufafanuzi kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	Anabainisha na kufafanua imani potofu na ukweli kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	Anabainisha na kufafanua kwa mifano kuhusu imani potofu na ukweli kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino) katika jamii.	
		e) Kubainisha huduma stahiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino)	Huduma stahiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino) zimebainishwa.	Anabainisha mafuta stahiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	Anabainisha mafuta na kofia stahiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	Anabainisha mafuta, kofia na miwani stahiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	Anabainisha mafuta, kofia, miwani na nguo stahiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino).	
		f) Kueleza tahadhari za kuchukua dhidi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni	Tahadhari za kuchukua dhidi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni zimeelezwa.	Anaeleza tahadhari mbili za kuchukua dhidi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni.	Anaeleza tahadhari tatu za kuchukua dhidi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni.	Anaeleza tahadhari nne za kuchukua dhidi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni.	Anaeleza tahadhari tano za kuchukua dhidi ya visababishi vingine vya ulemavu wa uoni na kutoa mifano halisi ya tahadhari kulingana na mazingira halisi.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
3.0 Kutumia sayansi ya jicho kuchambua hitilafu katika jicho	3.1 Kutumia sayansi ya jicho kubaini hitilafu za uoni	a) Kufafanua dhana ya hitilafu za uoni	Dhana ya hitilafu ya uoni imefafanuliwa.	Anafafanua maana ya hitilafu za uoni.	Anafafanua maana ya hitilafu za uoni kwa kuzitaja.	Anafafanua maana ya hitilafu za uoni kwa kuzitaja na kutoa mifano.	Anafafanua maana ya hitilafu za uoni kwa kuzitaja, kwa mifano na kuonesha madhara yake.	8
		b) Kubainisha hitilafu za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Dhana ya hitilafu za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni imebainishwa.	Anabainisha dhana ya hitilafu za uoni kwa mwanafunzi.	Anabainisha dhana ya hitilafu za uoni kwa mwanafunzi na kutoa mifano.	Anabainisha dhana ya hitilafu za uoni kwa mwanafunzi kwa mifano, michoro na michoro mguso.	Anabainisha dhana ya hitilafu za uoni kwa mwanafunzi kwa mifano, michoro, na michoro mguso na kwa kuhusianisha na mazingira halisi.	
		c) Kuchambua sababu za hitilafu za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Sababu za hitilafu za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimechambuliwa.	Anafafanua sababu moja ya hitilafu za uoni kwa mwanafunzi.	Anafafanua sababu mbili za hitilafu za uoni kwa mwanafunzi na kutoa mifano.	Anafafanua sababu tatu za hitilafu za uoni kwa mwanafunzi kwa kutoa mifano na madhara yake.	Anafafanua sababu nne za hitilafu za uoni kwa mwanafunzi kwa kutoa mifano, madhara yake na namna ya kuzuia.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	3.2 Kutumia sayansi ya jicho kurekebisha hitilafu za uoni	a) Kufafanua dhana ya urekebishaji wa hitilafu za uoni	Dhana ya urekebishaji wa hitilafu za uoni zimefafanuliwa.	Anafafanua maana ya urekebishaji wa hitilafu za uoni.	Anafafanua maana na umuhimu wa urekebishaji wa hitilafu za uoni.	Anafafanua maana, umuhimu, na njia za urekebishaji wa hitilafu za uoni.	Anafafanua maana, umuhimu, njia za urekebishaji wa hitilafu za uoni na kutoa mifano.	10
		b) Kubaini mbinu na vifaa vya urekebishaji wa hitilafu za uoni	Mbinu na vifaa vya urekebishaji wa hitilafu za uoni zimebainishwa.	Anabainisha mbinu mbili na urekebishaji wa hitilafu za uoni.	Anabainisha mbinu tatu na vifaa vya urekebishaji wa hitilafu za uoni.	Anabainisha mbinu nne na vifaa vya urekebishaji wa hitilafu za uoni na kutoa mifano.	Anabainisha mbinu tano na vifaa vya urekebishaji wa hitilafu za uoni na kutoa mifano kwa kuhusianisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.	
		c) Kueleza matumizi ya vifaa vya urekebishaji wa uoni	Matumizi ya vifaa vya urekebishaji wa uoni yameelezwa.	Anaeleza vifaa vya urekebishaji wa uoni kwa kuvitaja.	Anaeleza vifaa vya urekebishaji wa uoni kwa kuvitaja na sifa zake.	Anaeleza vifaa vya urekebishaji wa uoni kwa kuvitaja, sifa zake na kwa mifano.	Anaeleza vifaa vya urekebishaji wa uoni kwa kuvitaja, sifa zake, kutoa mifano na kutaja kazi zake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kufanya urekebishaji rahisi wa hitilafu za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Urekebishaji rahisi wa hitilafu za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni umefanywa.	Anafanya urekebishaji wa hitilafu za uoni kwa kubaini aina ya hitilafu.	Anafanya urekebishaji wa hitilafu za uoni kwa kubaini aina ya hitilafu na njia za kurekebishia hitilafu inayohusika	Anafanya urekebishaji wa hitilafu za uoni kwa kubaini aina ya hitilafu, njia na vifaa vya kurekebishia hitilafu inayohusika.	Anafanya urekebishaji wa hitilafu za uoni kwa kubaini aina ya hitilafu, njia na hatua za kurekebishia hitilafu inayohusika kulingana na mazingira.	
		e) Kubainisha mbinu za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Mbinu za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimebainishwa.	Anabainisha mbinu moja ya kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha mbinu mbili za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha mbinu tatu za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	Anabainisha mbinu nne za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na kutoa mifano kwa kuhusianisha na mazingira.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		f) Kueleza hatua za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni	Hatua tano za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni zimeelezwa.	Anaeleza hatua mbili za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	Anaeleza hatua tatu za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	Anaeleza hatua nne za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	Anaeleza hatua tano za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	
	3.3 Kutumia sayansi ya jicho kuchambua athari za uoni katika ujifunzaji	a) Kufafanua changamoto ya ujenzi wa dhana katika ujifunzaji	Changamoto nne za ujenzi wa dhana katika ujifunzaji zimefafanuliwa kwa kutumia hisimguso, kunusa, kusikia, kuonja na uoni (kwa wenye uoni hafifu).	Anafafanua changamoto moja ya ujenzi wa dhana katika ujifunzaji.	Anafafanua changamoto mbili za ujenzi wa dhana katika ujifunzaji.	Anafafanua changamoto tatu za ujenzi wa dhana katika ujifunzaji na kutoa mifano.	Anafafanua changamoto nne za ujenzi wa dhana kwa kutumia hisimguso, kunusa, kusikia, kuonja na uoni (kwa wenye uoni hafifu), kuelezea athari zake katika ujifunzaji na kutoa mifano.	6
		b) Kufafanua changamoto za ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Changamoto sita za ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimefafanuliwa.	Anafafanua changamoto mbili za ujifunzaji na kutoa mifano.	Anafafanua changamoto tatu za ujifunzaji na kutoa mifano.	Anafafanua changamoto tano za ujifunzaji na kutoa mifano.	Anafafanua changamoto sita za ujifunzaji na kutoa mifano kwa kuzingatia mazingira halisi.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kufafanua mbinu za kutatua changamoto za ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Mbinu za kutatua changamoto za ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimefafanuliwa.	Anafafanua mbinu mbili za kutatua changamoto za ujifunzaji wa mwanafunzi.	Anafafanua mbinu tatu za kutatua changamoto za ujifunzaji wa mwanafunzi.	Anafafanua mbinu nne za kutatua changamoto za ujifunzaji wa mwanafunzi.	Anafafanua mbinu tano za kutatua changamoto za ujifunzaji wa mwanafunzi.	
4.0 Kutumia mbinu za upimaji katika kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	4.1 Kutumia maarifa ya upimaji kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kueleza dhana ya ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Maana na umuhimu wa ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni vimebainishwa.	Anaeleza maana ya ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anaeleza maana na umuhimu wa ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anaeleza maana na umuhimu wa ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kwa kutoa mifano.	Anaeleza maana na umuhimu wa ubainishaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kwa kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	6

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kubainisha mbinu za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Mbinu za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimebainishwa.	Anabainisha mbinu moja ya kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha mbinu mbili za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kwa kutoa mifano.	Anabainisha mbinu tatu za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kwa kutoa mifano.	Anabainisha mbinu nne za kumbaini mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kwa kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	
		c) Kueleza hatua za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni	Hatua za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni zimeelezwa.	Anabainisha hatua mbili za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	Anabainisha hatua tatu za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	Anabainisha hatua nne za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	Anabainisha hatua tano za kuwatambua wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni.	
	4.2 Kutumia vifaa vya upimaji kuchunguza changamoto za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kubaini vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni vimebainishwa.	Anabanisha vifaa vya uchunguzi wa wa uoni.	Anabainisha vifaa vya uchunguzi wa uoni na kutoa mifano.	Anabainisha vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa kutaja majina na kutoa mifano.	Anabainisha vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa kutaja majina na mifano na kueleza matumizi yake.	6

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuelezea vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Vifaa sita vya uchunguzi wa uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni vimefafanuliwa.	Anafafanua vifaa vya uchunguzi wa uoni.	Anafafanua vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa kutaja vifaa viwili.	Anafafanua vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa kutaja vifaa vinne.	Anafafanua vifaa vya uchunguzi wa uoni kwa kutaja vifaa sita na kueleza matumizi yake.	
		c) Kubainisha changamoto za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Changamoto za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimebainishwa.	Anabainisha changamoto mbili za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha changamoto nne za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha changamoto tano za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na kueleza athari zake.	Anabainisha changamoto sita za uoni kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni, kueleza athari zake na kutoa mifano.	
	4.3 Kutumia mbinu za upimaji katika kutoa afua stahiki za kielimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kufafanua dhana ya afua stahiki za kielimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Maana, aina na umuhimu wa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimefafanuliwa.	Anafafanua maana za afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anafafanua maana na aina za afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anafafanua maana, aina na umuhimu wa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	8

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kubainisha njia za kutoa afua stahiki za kielimu kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Njia za kutoa afua stahiki za kielimu kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimebainishwa.	Anabainisha njia za kutoa afua stahiki za kielimu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha njia za kutoa afua stahiki za kielimu kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni.	Anabainisha njia za kutoa afua stahiki za kielimu kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni na kutoa mifano.	Anabainisha njia za kutoa afua stahiki za kielimu kulingana na mahitaji ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kwa kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira ya ujifunzaji.	
		c) Kubainisha njia za kutatua changamoto za utoaji wa afua stahiki	Njia za kutatua changamoto za utoaji wa afua stahiki zimebainishwa.	Anabainisha njia za kutatua changamoto za utoaji wa afua stahiki.	Anabainisha njia za kutatua changamoto za utoaji wa afua stahiki na kutoa mifano.	Anabainisha njia za kutatua changamoto za utoaji wa afua stahiki, kutoa mifano na kuhusianisha na uhitaji.	Anabainisha njia za kutatua changamoto za utoaji wa afua stahiki, kutoa mifano, kuhusianisha na uhitaji na kupima matokeo ya afua hizo.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	4.4 Kutoa afua stahiki kwa wanafunzi waliobainika kuwa na hali ya ulemavu wa uoni (kutoa rufaa, kupendekeza huduma kulingana na mahitaji, kurekebisha maeneo, vifaa saidizi na hali)	a) Kuandaa rufaa kulingana na changamoto za uoni kwa wanafunzi waliobainika	Rufaa kulingana na changamoto za uoni kwa wanafunzi waliobainika zimeandaliwa.	Anaandaa rufaa kulingana na changamoto za uoni kwa wanafunzi waliobainika kwa kutaja hatua za kufuata.	Anaandaa rufaa kulingana na changamoto za uoni kwa wanafunzi waliobainika kwa kuzitaja hatua za kufuata na kuzielezea.	Anaandaa rufaa kulingana na changamoto za uoni kwa wanafunzi waliobainika kwa kuzitaja hatua za kufuata, kuzielezea na kutoa mifano.	Anaandaa rufaa kulingana na changamoto za uoni kwa wanafunzi waliobainika kwa kuzitaja hatua za kufuata, kuzielezea, kutoa mifano na kuhusianisha na mazingira.	10
		b) Kueleza ushauri na unasihi unaotakiwa kutolewa kwa wanafunzi, wazazi na walezi wa wanafunzi waliobainika kuwa na changamoto za uoni	Ushauri na unasihi unaotakiwa kutolewa kwa wanafunzi, wazazi na walezi wa wanafunzi waliobainika kuwa na changamoto za uoni vimeelezwa.	Anaeleza ushauri na unasihi unaotakiwa kutolewa kwa wanafunzi waliobainika kuwa na changamoto za uoni.	Anaaeleza ushauri na unasihi unaotakiwa kutolewa kwa wanafunzi, wazazi na walezi wa wanafunzi waliobainika kuwa na changamoto za uoni.	Anaeleza ushauri na unasihi unaotakiwa kutolewa kwa wanafunzi, wazazi na walezi wa wanafunzi waliobainika kuwa na changamoto za uoni na kutoa mifano.	Anaeleza ushauri na unasihi unaotakiwa kutolewa kwa wanafunzi, wazazi na walezi wa wanafunzi waliobainika kuwa na changamoto za uoni kwa kutoa mifano na kuhusiana na mazingira.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kueleza athari za ulemavu wa uoni (kielimu, kijamii, kisaikolojia, kiuchumi)	Athari nne za ulemavu wa uoni (kielimu, kijamii, kisaikolojia, kiuchumi) zimeelezwa.	Anaeleza athari mbili za ulemavu wa uoni (kielimu na kijamii).	Anaeleza athari tatu za ulemavu wa uoni (kielimu, kijamii na kisaikolojia).	Anaeleza athari nne za ulemavu wa uoni (kielimu, kijamii, kisaikolojia na kiuchumi).	Anaeleza athari nne za ulemavu wa uoni (kielimu, kijamii, kisaikolojia na kiuchumi) na kutoa mifano kulingana na mazingira yanayomzunguka.	

Orodha ya Machapisho

Blasch, B. B., Welsh, R. L., & Wiener, W. R. (1997). *Foundations of orientation and mobility* (2nd ed.). New York, United States of America: AFB Press.

Inclusive Development Promoters and Consultants. (2016). *Kamusi elekezi ya ulemavu, kingereza–kiswahili.* Dar es Salaam, Tanzania: Nesmap Printing Technology.

Gay, M. M., Stecker., N. A., & Katz, J. (1998). *Central auditory processing disorders, mostly management.* New York, United States of America: Pearson Education.

Leigh, R. J., & Zee, D. S. (2015). *The neurology of eye movements* (5th ed.). Oxford, England: Oxford University Press.

Tanzania Institute of Education. (2012). S*yllabus for Certificate in Special Needs Education*. Dar es Salaam, Tanzania: Ministry of Education and Vocational Training.

Punani, B., & Rawal, N. (2000). *Handbook on visual impairment.* Ahmedabad, India: The Blind People's Association.